Hii ni hali ya kuwa kiume au kike. Yaani, sifa za kibiolojia kati ya wanaume na wanawake. Kwa mfano, wanaume wana ndevu lakini wanawake wana matiti.	Wajibu na majukumu wanaopewa wanaume na wanawake (wavulana na wasichana) Kwa mfano, wanawake hushughulika na utunzaji wa nyumba na watoto lakini wanaume hufanya kazi na kulinda familia.


Ni sawa kote duniani. Yaani, kama wewe ni mwanaume / mwanamke katika Bonde la Ufa, wewe bado ni mwanamume / mwanamke hata ukienda Mkoa wa Kati.	Inatofautiana kulingana na utamaduni, eneo la kijiografia, utajiri, dini na kadhalika. Kwa mfano, kazi ya ujenzi wa nyumba ni wajibu wa mwanaume miongoni mwa Wakikuyu na Wakalenjin lakini miongoni mwa Wamaasai ni wajibu wa wanawake.
Haiwezi kubadilika. Hii inamaanisha kuwa wanaume hawawezi kufanya kazi za kibiojia za wanawake (Kwa mfano kupata ujauzito na kunyonyesha). Vile vile, wanawake hawawezi kufanya kazi za kibiologya za wanaume. Kwa mfano, kutengeneza mbegu za uzazi na kufanya wanawake washike mimba.	Hubadilika muda unavyopita. Kwa mfano, katika tamaduni nyingi, wanawake walilazimika kubaki nyumbani lakini siku hizi wengi wao huajiriwa na kutunza familia yao. Vile vile, wanaume wamechukua kazi ambazo zamani jamii ilidhania kuwa za wanawake kama uuguzi na ususi.
Kibiologya / uliyopewa na Mungu	Hupewa na jamii.

Ufafanuzi wa masuala muhimu ya jinsia

Wajibu wa kijinsia: Huu ni wajibu, tabia na majukumu waliyopewa wanawake na wanaume, kulingana na jinsi jamii inawatarajia kutenda. Majukumu haya yanaweza kuwa tofauti kulingana na umri, mahali, kabilia, utajiri, dini, mazingira tofauti ya kiuchumi na kisiasa na hubadilika na muda. Kwa mfano, mionganoni mwa jamii ya Wamaasai kujenga nyumba ni jukumu la mwanamke lakini katika jamii ya Wakikuyu ni jukumu la mwanaume.



Usawa wa Jinsia: Hii inamaanisha fursa sawa ya nafasi za kazi, rasilimali na huduma kwa wasichana / wavulana na wanawake / wanaume bila kubaguliwa.




Usawazishaji wa Jinsia: Hii inamaanisha usambazaji wa fursa, rasilimali na faida kati ya wasichana / wanawake na wavulana / wanaume. Mifano ni sheria ya kijinsia ya thuluthi mbili ya uongozi katika bunge au kuwasajili wasichana katika vyuo vikuu vya umma wakiwa na alama za chini kuliko wavulana. Hii ni kwa sababu, zamani, wasichana na wanawake walinyimwa haki na hivyo basi, kuifanya muhimu kutafuta njia za kuwapa haki zao.

Ubaguzi wa kijinsia: Hii inahusu jinsi tofauti ya kumtendea mtu kwa sababu ya jinsia yake. Kwa mfano wazazi kukataa kuwaelimisha wasichana au kuwapa mali.


Mfumo dume: Hii inamaanisha “uongozi wa baba” na ni mfumo wa jamii unaowaweka wanaume katika nafasi bora huku wanawake wakiwekwa katika nafasi ya chini katika jamii. Hii ni kawaida sana duniani kote.

Mfumo kike: Hii inamaanisha “uongozi wa mama” na ni kinyume cha mfumo dume. Hata hivyo, katika jamii ambayo ina mfumo kike, ni katika maswala kama kuwapa watoto majina tu, lakini nguvu halisi bado ipo kwa wanaume.

Uume: Hii ni hali ya kuwa mvulana / mwanaume katika jamii fulani. Baada ya kuzaliwa kama mtoto wa kiume, jamii hufafanua tabia yako na pia kutia ndani yako imani na mitazamo fulani. Pia, inaeleza jinsi unapaswa kuhusiana na wewe mwenyewe, watu wa jinsia sawa, pamoja na wale wa jinsia tofauti. Baadhi ya sifa ambazo huhuishwa na uume ni kama vile kuwa na nguvu, kutumia fujo na kadhalika.



Uke: Hii ni hali ya kuwa msichana / mwanamke katika jamii fulani. Baada ya kuzaliwa kama mtoto wa kike, jamii hufafanua tabia yako na pia kutia ndani yako imani na mitazamo fulani. Pia, inaeleza jinsi unapaswa kuhusiana na wewe mwenyewe, watu wa jinsia sawa, pamoja na wale wa jinsia tofauti. Sifa ambazo huhushishwa na uke ni kama vile urembo, uvumilivu, wema, utulivu na kadhalika.



Uwezeshaji: Hizi ni njia za kuboresha maisha ya watu kwa kuwapa uwezo wa kujifanya vitu wao wenyewe. Kwa mfano, kuwapa wanawake na wasichana elimu, maarifa, ujuzi na mafunzo ili kuwawezesha kufanya maamuzi ya busara na kupata ajira. Kuwasaidia wanaume kutambua kwamba wao wanaweza



kukabiliana na uume wao bila kuwadhuru wengine, pia ni aina ya uwezeshaji.

Ni nini maana ya ujenzi wa kijamii wa jinsia?

Hii ni njia ambayo jamii hutufundisha jinsi ya kuwa wavulana / wasichana na wanaume / wanawake. Hii husukumwa na sababu mbali mbali kama tamaduni, mahali tunamoishi, dini yetu, utajiri wetu na kadhalika.

Mahali ambapo ujenzi huu hufanyika ni kama:

a) Familia / mazingira ya nyumbani

Hii ni sehemu ya kwanza ambapo ujenzi wa kijamii wa jinsia huanza. Tangu kuzaliwa, watoto wavulana na wasichana hutendewa tofauti. Wakati wanakua, wavulana hupewa




majukumu ambayo huwaandaa kwa majukumu yao ya baadaye kama waume na baba. Majukumu haya ni kama kuwa viongozi wa familia, walinzi na kadhalika. Wasichana kwa upande wao, hutayarishwa kuwa wake na mama, hivyo basi, hufundishwa kupika, kusafisha nyumba, utunzaji wa ndugu na kwa jumla kufanya kazi za nyumbani.

b) Shule / elimu

Tabia na desturi za kijinsia zilizoanzishwa nyumbani, huendelezwa shulenii.


Mfano mzuri ni majukumu ambayo wanafunzi katika shule za mseto hupewa, ambapo wavulana hupata uongozi na majukumu makuu kama kuwa viranja wakuu huku wasichana wakichukua majukumu ya kuwa manaibu au wasaidizi wao.



Wanafunzi pia huwaiga walimu; wao huona walimu wa kike katika sanaa na walimu wa kiume katika sayansi na hili hutoa ujumbe mkubwa. Wakati mwingine walimu pia huathiri mawazo ya wanafunzi wao kwa kuhamasisha wavulana kufanya kazi kwa bidii na kuwa na mafanikio na kuwakubalia wasichana wasifanye kazi kwa bidii kwa vile wao huolewa na kutunzwa na waume zao. Kwa bahati nzuri, hali hii inabadilika hata kama ni pole pole. Shule zetu na vituo vyta elimu zinatafaa kuwalea wavulana na wasichana bila ubaguzi ili wote wafanikiwe.

c) Dini

Biblia yenye wadudu haibagi jinsia na kwa kweli huwawezesha sana wanawake. Hata hivyo, kama katika taasisi zote za jamii, uongozi wa makanisa unatawaliwa na wanaume na maelezo ya maandiko basi husukumwa na mfumo dume ambao umekita mizizi katika utamaduni. Maandiko mengi ya Biblia huelezwa



kwa njia ambazo huwaonea wanawake lakini wakati mwingi hakuna uwajibikaji wa wanaume kwa matendo yao.

UKATILI WA KIJINSIA

Ukatili: Hii ni matumizi yoyote ya nguvu dhidi ya mtu inayosababisha madhara, maumivu au mateso.

Ukatili wa kijinsia: Hiki ni kitendo chochote kinachosababisha (au kinatishia kusababisha) madhara, maumivu au mateso ambayo huelekezwa mwanamme au mwanamke kwa sababu ya jinsia yake. Wakati mwingine wanaume na wavulana hutendewa aina fulani ya ukatili wa kijinsia, lakini wanawake na wasichana hutendewa zaidi.

Ukatili dhidi ya wanawake: Hivi ni vitendo vyovyote vinavyosababisha (au vinatishia kusababisha) madhara, maumivu au mateso ambayo huelekezwa wanawake kwa sababu wao ni wanawake.

Ukatili dhidi ya wanaume: Hivi ni vitendo vyovyote vinavyosababisha (au vinatishia kusababisha) madhara, maumivu au mateso ambayo huelekezwa wanaume kwa sababu wao ni wanaume.

Ukatili wa majumbani: Hivi ni vitendo vyovyote vinavyosababisha (au vinatishia kusababisha) madhara,

maumivu au mateso ambayo huelekezwa kwa mtu katika uhusiano wa karibu kwa mfano mume na mke, watu ambao wanachumbiana, watu ambao wana mtoto pamoja na kadhalika. Aina hii ya ukatili hutokea hasa katika mazingira ya nyumbani / jamaa lakini ni uhusiano baina ya watu ambao huufafanua kuwa kama wa kinyumbani. Ukatili unaofanywa dhidi ya mtu katika uhusiano wa karibu uliopita (kwa mfano, mume wa zamani / mke wa zamani) bado unastahili kuangaziwa kama ukatili wa majumbani.

Mtekelezaji: Huyu ni mtu anayetenda kitendo cha unyanyasaji au ukatili dhidi ya mtu mwingine. Anaweza kuwa mgeni au mtu mwenye uhusiano wa karibu/anayejulikana kwa mwaathirika/mnusura.

Mwathiriwa/Mnusura: Huyu ni mtu ambaye amefanyiwa kitendo cha ukatili. Mnusura hutumiwa kuliko mwathiriwa kwa sababu yeye amepitia ukatili wa kijinsia na kupokea nguvu ya kindani na uamuzi wa kuishi.

AINA YA UKATILI WA KIJINSIA

Zifuatazo ni aina fulani za ukatili wa kijinsia na mifano yao:

Dhuluma ya kimapenzi

Hii inamaanisha kitendo cha asili ya ngono dhidi ya mtu kinyume na ridhaa yake au ambapo mtu anakubali lakini yeye hana uwezo (kwa mfano akiwa na umri wa miaka chini ya 18

au wakati ambapo mtu hutishwa). Jaribio la kitendo kama hiki linastahili kuangaziwa kama ukatili wa kijinsia na kuadhibiwa kisheria. Mifano ya ukatili wa kijinsia ni ubakaji (kwa watu wazima), kunajisi (kwa watoto chini ya miaka 18), mahusiano ya kingono kati ya ndugu wa karibu na kulawiti.

Ukatili wa kimwili

Hii inaweza kufanywa na au bila matumizi ya silaha kama visu, majembe au mapanga. Mifano ni kama kukwaruzwa, kuuma, kusukuma, kupiga, kunyongwa, kuchomwa na kupiga ngumi.

Ukatili wa kiuchumi

Aina hii ya ukatili hutumiwa na wahusika kama njia ya kudhibiti mazingira ya nyumbani. Mifano ni kunyimwa au kudhibitiwa matumizi ya rasilimali za familia kama chakula, fedha, mavazi, gari na hata wakati mwingine, kupinga mtu kwenda kufanya kazi na kuchukua au kudhibiti mapato yake.


Ukatili wa kisaikolojia na wa kihisia

Makundi haya mawili ya ukatili huhusisha vitendo vya kusababishia mateso ya kiakili na ya kihisia.



Mifano ni vitisho vya vita, kutukana, kutengwa, kutumia watoto ili kutisha mwingine na ukimya.

Ukatili wa kitamaduni: Huu huhusisha tamaduni zinazoibua ukiukwaji wa haki za wale wanaoangaziwa. Hii ni kama ukeketaji wa wanawake (FGM), ndoa za mapema, ndoa za kulazimishwa, mjane kurithiwa/ kupokonywa urithi na dhuluma kwa wajane.



WATEKELEZAJI WA UKATILI WA KIJINSIA

Wengi hufikiria kuwa watekelezaji wa ukatili wa kijinsia ni watu ambao hawajulikani. Ingawa hii inaweza kuwa kweli kwa kiwango fulani, ukweli ni kwamba vitendo vingi vya ukatili wa kijinsia hufanywa na watu wa karibu na manusura / waathirika. Mara nyingi wahusika ni watu ambao waathirika huwaamini na kuwategemea kwa msaada na ulinzi. Wao ni kama:

- Waume / marafiki wa kiume
- Jamaa/ familia ya karibu / Marafiki / Majirani
- Watu wenye ushawishi mkubwa katika jamii
- Wanasiasa/ Walimu / Viongozi wa kidini / Waajiri

NINI HUSABABISHA UKATILI WA KIJINSIA?

Mambo mengi yanaweza kusababisha ukatili wa kijinsia lakini uchunguzi wa masuala haya yote huonyesha ya kwamba kiini cha shida hii ni uwezo na utawala. Uwezo ni mzuri unapotumiwa kwa njia ipasayo kwa mfano kufanya maamuzi yanayoathiri maisha yetu. Huu uwezo pia unatuwezesha kushirikiana na wengine. Hatutishwi na wengine na hatuna shida kuwasikiliza au kufanya maamuzi pamoja. Ni wakati ambapo tunahisi kuwa hatuna uwezo ambapo shida hujitokeza. Tunatumia ule uwezo tuko nao vibaya kwa kuwadhulumu wale ambao hawana uwezo wa kutosha. Huu utumiaji vibaya wa nguvu ndio sababu kuu ya ukatili wa kijinsia na hutokana na hisia ya kutokuwa na uwezo. Watu ambao hawana uwezo mara nyingi huhisi kama hawana maana na hujaribu kujipea nguvu na maana kwa kuwadhulumu wengine. Ni muhimu kuelewa kwamba mambo haya yanahusisha ukatili wa kijinsia kwa

jumla hata kama mhusika ni mwanaume au mwanamke. Mambo yafuatayo yanatoa maelezo zaidi ;

Tabia na hisia za kipekee za mtu: Watendaji wa ukatili wa kijinsia huhisi kuwa wao ni duni na hawajiamini. Kama ilivyotajwa hapo juu, ni hisia ya kutokuwa na uwezo inayowasukuma wadhulumu wengine ili wahisi wao ni watu wa maana.

Sababu za kiuchumi : Watendaji wengi wa ukatili wa kijinsia hasa wale ambao wako katika uhusiano wa karibu hutaka kuhakikisha kuwa waathiriwa wanawategemea kabisa. Njia nzuri ya kufanya hivi ni kwa kuwadhibiti kiuchumi kama vile kuwanyima nafasi za kazi au biashara, elimu bora au pia uhusiano unaonekana kuwajenga waathiriwa. Kuna matukio mengi ambapo waume wanawakataza wake wao kufanya kazi au kurudi shulenii. Mume anapohakikisha kuwa mke wake anamtegemea kabisa, ni rahisi kudhibiti mambo anayofanya na mahali anapoenda. Hii inamwezesha mume kumtawala mke wake kwa kuhakikisha hafanyi kitu au kuenda popote bila ruhusa.

Sababu za kihisia /kisaikolojia : Kwa kawaida, watendaji wa dhuluma ya kijinsia hawajiamini. Kwa mfano, mume husika huhisi kama yeye si “mwanaume kamili” na huogopa kuwa mke wake atapata mwanaume bora zaidi (tukio hilo ni sawa na jinsi wanawake wengine hushuku kila wakati kuwa waume wao si waaminifu). Ni kawaida kwao kuwalamu wake au waume wao kuwa wadanganyifu na hizi shauku hutumiwa kuhalalisha dhuluma yao. Ili kuzuia mke kuwa mdanganyifu,

mhusika hutumia utengaji na huamua ni uhusiano upi unaoruhusiwa na upi unaokatazwa. Vile vile, mwanamke ambaye hajiamini anaweza kudhulumu mumewe kwa matusi au pia dhuluma ya kihisia. Hii ni njia nyingine ya mtendaji kudhibiti na kumwonyesha mwathiriwa nguvu yake.

Sababu za kitamaduni : Kuna aina nyingine za ukatili wa kijinsia zinazosababishwa na imani na mazoea ya kitamaduni. Kwa mfano, ukeketaji, urithi wa wake, usafishaji wa wajane, ndoa ya watoto, ndoa ya lazima, upigaji wa wake na kunyima wanawake haki za mali na urithi. Kwa hiyo mifano yote, uwezo na utawala ndizo sababu kuu. Kwa mfano, ukeketaji ni njia ya kupunguza nguvu za kike ili wanawake wawe waaminifu kwa waume wao. Kwa upigaji wa mke, wanaume wengine huamini kuwa wanawake ni kama watoto na wanafaa kupigwa kama njia ya kuwapa adabu au kuonyesha mapenzi. Katika ndoa, ulipaji wa mahari unatatiza shida hii zaidi kwa sababu inawafanya wanawake waonekane kama bidhaa “zilizonunuliwa” na hivyo basi, ni mali ya waume wao. Ni rahisi kuona jinsi utamaduni hutumiwa kuhalalisha matumizi mabaya ya nguvu kuwadhibiti na kuwadhulumu wanawake, wanaonekana kama duni.

Sababu za kifamilia : Mtu anayelelewa katika familia yenyε ukatili wa kijinsia mara nyingi huwa mtendaji wa ukatili. Ingawa, hii haifanyiki kila mara kwani kuna watu ambao huepukana na vita baada ya kuishuhudia katika familia zao, kuna wale ambao huiga tabia za wazazi wao bila kuelewa sababu. Hii inaeleza sababu wasichana wengine huolewa na wanaume

wakatili kama baba zao au wavulana huoa wanawake wakatili kama mama zao. Ni muhimu kwa wanawake wanawake wanaodhulumiwa katika ndoa waelewe hivi. Wanafaa kujiuliza ikiwa wanawaletea watoto wao madhara zaidi kuliko mema.

Ili kuelewa vile uwezo na utawala zinachangia ukatili wa kijinsia, ni muhimu kufahamu kuwa hata kama mara nyingi waathiriwa ni wanawake, wakati mwingine ukatili wa kijinsia hutendwa dhidi ya wanaume. Aina za vita dhidi ya wanaume zinafanana na zile dhidi ya wanawake. Lakini mbali na wanawake kuwa watendaji wa ukatili wa kijinsia, wanaume pia hutenda ukatili huu dhidi ya wanaume wenzao. Mfano mzuri ni dhuluma ya kimapenzi dhidi ya wanaume wenzao. Si rahisi kujua kama upungufu wa kesi zilizoripotiwa na wanaume ni kwa sababu matukio ya dhuluma hii ni chache au ni kwa sababu wanaume hawakubaliwi kuongea kuhusu shida zao. Mwanaume anapodhuluiwa na mwanamke, si rahisi kumwambia mtu mwingine kwani anaonekana dhaifu machoni mwa wengine. Hivyo basi, pengine kuna wanaume wengi wadhulumiwa na wake wao bila kusema chochote. Dhuluma ya kimapenzi inapotendwa na mwanaume dhidi ya mwanaume mwingine, aibu na unyanyapaa huwazuia kuzungumza kuhusu ukatili huo.

Kwa ufupi, chanzo kuu cha ukatili wa kijinsia ni wakati ambapo mtu huhisi hana uwezo wa kujitunza. Watendaji wa ukatili wa kijinsia ni watu wanaohisi kuwa hawana maana na hujaribu kupata tena nguvu yao kuitia vita wawe wanawake au wanaume. Pia, haijalishi kama vita ni vya kupigana, kisaikolojia

au vya kimapenzi. Watu ambao wanajiamini hawahitaji kuonyesha ubora wao kupitia vita. Ni muhimu kuelewa ya kwamba wanaume hawazaliwi wakiwa wakatili na si wanaume wote wakatili. Kama vile kuna wanaume wengine wakatili vile vile kuna wanawake wakatili pia. Wanaume pia wanafaa kuelewa kuwa wanawake huhisi uchungu wa waathiriwa kwa jinsi sawa na wanaume. Hivyo basi hakuna mtu aliye na haki ya kudhulumu mwengine, awe mwanaume au mwanamke.

ATHARI ZA UKATILI WA KIJINSIA

Madhara kwa mwathiriwa Kimwili

- Majeraha
- Ulemavu
- Matatizo ya afya (kwa mfano magonjwa ya roho vidonda za tumbo na kadhalika)
- Matatizo ya ngono na uzazi afya (Kwa mfano magonjwa ya zinaa, ukimwi na kadhalika)
- Kifo

Kisaikolojia

- Wasiwasi
- Hofu / ukosefu wa usalama / Kujichukia
- Kutoamini wengine
- Kutokuwa na uwezo wa kutia makini
- Kutokuwa na uwezo wa kuhusiana na watu wengine/ upweke
- Mawazo mazito
- Ulevi na matumizi ya dawa za kulevya / Kutojamini
- Kujilaumu

- Mawazo ya kijiua/ tabia za kutaka kijiua / majaaribio ya kijiua
- Ugonjwa wa akili

Kijamii

- Kujitenga
- Lawama / kukataliwa na mpenzi, jamaa na jamii
- Unyanyapaa
- Kutokuwa na uwezo wa kushiriki katika shughuli za kijamii
- Hofu ya siku za baadaye au kuenda katika maeneo ya umma
- Kuvunjika kwa familia
- Ukosefu wa uwezo wa kufanya maamuzi
- Kukosa uwezo wa kujisaidia
- Kutoweza kufanya kazi yoyote kwa mfano, kujitunza au kuwalea watoto.

Kiuchumi

- Kupoteza kazi kutokana na utoro, kushindwa kutekeleza wajibu na hofu, ukosefu wa kujiamini
- Utegemezi kwa mtekelezaji ambaye hudhibiti rasilimali za familia
- Umaskini

Athari kwa watoto

- Kutojiamini
- Wasiwasi
- Kujitenga/Kujilaumu
- Vita kwa wengine

- Ulevi na matumizi ya dawa za kulevyta na aina nyingine za tabia zisizoambatana na jamii
- Ukosefu wa mahitaji ya kimsingi
- Kuacha masomo/Ukahaba wa watoto

Watoto kama hao pia huwa na hatari ya kuwa watekelezaji wa ukatili wa kijinsia. Wale ambaao huwa wahusika hurudia matendo yale ambayo walishuhudia nyumbani.

Kuna wale ambaao huuona ukatili huo kama jambo la kawaida baada ya kushuhudia yale yanatokea nyumbani. Hawa huo au huolewa na watu ambaao ni sawa na wazazi wao watesi kwani ni kile wanachokiona kama kawaida. Hii inaeleza kwa nini baadhi ya wasichana ambaao baba zao walikuwa watesi huolewa na wanaume ambaao ni kama baba zao.

Athari kwa watekelezaji

- Hisia za hatia
- Upweke
- Kutengwa na familia na jamii
- Kupunguka kwa uwezo kutokana na ukosefu wa mazingira mazuri nyumbani
- Kupunguka kwa mapato kwa mfano, kutumia pesa kulipabili za hospitali
- Unywaji wa pombe na kutumia madawa ya kulevyta
- Kuvunjika kwa familia
- Wasiwasi
- Kujiua (ama kujaribu kujiua)

SHERIA INASEMA NINI KUHUSU UKATILI WA KIJINSIA?

Ukatili wa kijinsia ni ukiukaji wa haki za binadamu na aina nyingi za ukatili wa kijinsia zinaweza kuadhibiwa na sheria. Kuna sheria ambazo zinafaa kutulinda dhidi ya vitendo vingine vyta ukatili wa kijinsia. Sheria nyingine huonyesha ni haki gani wanaume, wanawake na watoto wanastahili kuwa nazo, na hizo haki hazifai kukiukwa. Nyingine hufafanua makosa yanayofanywa kuitia vitendo tofauati vyta ukatili wa kijinsia na hueleza adhabu ya kila kosa. Hizi sheria ni kama:

Katiba: Hii ndio sheria kuu nchini na hueleza kuwa wanaume na wanawake ni sawa kulingana na sheria na wana haki sawa ya kufaidika na kulindwa na sheria. Hii inamaanisha kuwa kila mtu ana haki ya nafasi sawa katika nyanja za kisiasa, kitamaduni na kijamii. Wanaume na wanawake wana haki ya kulindwa dhidi ya vita, kuteswa, matendo katili au kinyama. Hii inamaanisha ya kwamba katiba inawalinda wanaume na wanawake dhidi ya ukatili wa kijinsia.

Kanuni ya Adhabu (Penal Code): Hii sheria inafafanua makosa yanayovunja sheria na pia adhabu zao. Mifano ya vitendo vyta ukatili wa jinsia yanayofafanuliwa katika Kanuni ya Adhabu ni:



- Shambulio – Hii inahusu matendo yanayo muumiza mtu kimwili kwa mfano kuchapwa, kupigwa kofi, kuchomwa na kadhalika.
- Makosa yanayokiuka maumbile - Haya ni kama kulawiti (matendo ya kimapenzi kinyume na utaratibu wa maumbile), matendo ya kimapenzi yanayohusu wanyama na matendo machafu kati ya wanaume.

Sheria ya makosa ya kimapenzi (Sexual Offences Act): Hii ni sheria inayofafanua matendo ya dhuluma ya kimapenzi. Kwa mfano, ubakaji au jaribio la ubakaji (ikiwa mwathiriwa ni mtu wa miaka 18 na zaidi), unajisi au jaribio la unajisi (ikiwa mwathiriwa ni mtu wa miaka chini ya 18) na matendo ya kimapenzi baina ya watu wa familia moja)

Sheria ya watoto (The Children Act): Hii ni sheria inayowalinda watoto (wavulana na wasichana) dhidi ya dhuluma ya kisaikolojia, kupuuzwa au aina yoyote ile ya unyanyasaji kama vile kuuzwa na kutekwa nyara. Hii sheria pia inawalinda watoto dhidi ya ukeketaji, ndoa ya watoto au mazoea mengine ya kitamaduni yanayoleta madhara katika maisha ya mtoto anapokua.

Sheria inayozuia ukeketaji (Prohibition of Female Genital Mutilation Act): Hii sheria inasema ya kwamba ukeketaji ni kinyume na sheria. Ni makosa kutenda ukeketaji, kuruhusu mwingine atekeleze ukeketaji, kuruhusu nyumba au jengo lako litumiwe kuitekeleza au kutoripoti tukio la ukeketaji baada ya kujua.

Sheria ya ulinzi dhidi ya ukatili wa nyumbani (Protection Against Domestic Violence Act): Inawalinda watu ambao wako ama waliokuwa katika uhusiano wa karibu dhidi ya ukatili. Uhusiano huu ni kama baina ya mume na mke (au mume na mke wa zamani), watu wanaosuhubiana au kuishi pamoja nyumbani. Baadhi ya makosa yanayotajwa katika sheria hii ni ndoa ya watoto, ukeketaji, ndoa ya lazima, urithi wa wake, maingiliano ya jamaa na vita vya kimapenzi katika ndoa.

Sheria ya urithi (Law of Succession Act): Sheria hii inalinda haki ya urithi ya watoto wa kiume na kike. Ni muhimu kufahamu kuwa watoto wa kiume na kike wana haki ya kurithi kulingana na mahitaji na uwezo wao. Mali ya mume au mke inafaa kurithiwa na watoto wao kwa hivyo mwanamke anayerithi kutoka kwa wazazi wake harithi mara mbili kwa sababu hafai kurithi kutoka kwa mume.

Hatua za kufuatwa katika kesi ya ubakaji au kunajisi.


- ❖ Kumshauri mwathiriwa kutooga au kubadilisha nguo kwani hii inaweza kuathiri ushahidi. Ili kuhifadhi ushahidi, sampuli zikusanywe kati ya masaa 24 na 72 (siku 1-3). Kama mwathiriwa atabadili nguo, anastahili kuziweka katika mfuko usio wa plastiki ili kuhifadhi ushahidi.
- ❖ Kupata matibabu. Daktari anatarajiwa kujaza fomu ya **Post Rape Care (PRC)** inayotoa maelezo ya matibabu ya mwathiriwa. Fomu ya PRC inaweza kujazwa na daktari, afisa wa kliniki au muuguzi.

- ❖ Baada ya matibabu, ripoti matukio katika kituo cha polisi kilicho karibu. Polisi wanapaswa kumpa mwathiriwa fomu ya P3 ambayo lazima ijjazwe na daktari. Baada ya fomu ya P3 kujazwa irejeshwe katika kituo cha polisi kwa ajili ya ulinzi. Hii hutumika kama ushahidi wakati kesi inapelekwa mahakamani.
- ❖ Mara polisi wamalizapo kukusanya ushahidi, wanatarajiwa kumkamata mtuhumiwa na kumpeleka mahakamani chini ya masaa 24.

TUNAWEZA KUFANYA NINI ILI KUZUIA UKATILI WA KIJINSIA?

Zifuatazo ni njia kadhaa ambazo tunaweza kutumia kuzuia tukio la ukatili wa kijinsia katika jamii zetu:


- a) Kuelimisha wanajamii juu ya ukatili wa kijinsia na jinsi ya kuuzuia. Hii inaweza kufanyika katika makanisa, mikutano ya familia na mikusanyiko ya jamii kama mabaraza.
- b) Ku f a n y a kazi pamoja na miundo rasmi, isiyo rasmi na mikusanyiko ya jamii. Kwa mfano



utawala wa eneo fulani na polisi ili kuzuia ukatili wa kijinsia.

- c) Kuwa mfano wa kuigwa. Mabingwa dhidi ya ukatili wa kijinsia wanapaswa kuongoza kwa mfano na kufanya mazoezi katika maisha yao wenyewe kwa yale wanayohubiri na kuyafunza.
- d) Kuwafunza watoto kuheshimu kila mmoja katika jamii.

TUNAWEZAJE KUKABILI IPASAVYO UKATILI WA KIJINSIA



UNAPOTOKEA?

Hatua za kukabiliana na ukatili wa kijinsia

- ❖ Kupokea kesi za ukatili wa kijinsia na kuzikabili ipasavyo. Tunafaa kuwa makini, bila kuegemea upande wowote. Hii itahakikisha waathirika kuripoti kesi za ukatili wa kijinsia. Ambapo kesi zilizoripotiwa zimepita kiwango chako, mwelekeze mwathiriwa kwa mamlaka ya juu husika kwa mfano, chifu au polisi.
- ❖ Elekezo kwa msaada mwafaka. Kulingana na asili na



aina ya ukatili wa kijinsia, mwathiriwa ahusishwe na vyanzo vinginevyo vya msaada:

- o **Msaada wa kimatibabu**- hii inahusisha hospitali, zahanati na vituo vya kiafya katika jamii kwa ajili ya kesi ambayo inahitaji matibabu.

- **Msaada ya kisheria** baadhi ya kesi za ukatili wa kijinsia zinahitaji msaada wa kisheria. Waathirika wanahitaji kuwa na uhusiano na wale ambao wanaweza kutoa msaada. Kwa mfano maafisa wa watoto na vile vile maafisa wanaohusika na masuala ya jinsia.
- **Msaada ya kiutawala** - Hii ni pamoja na chifu, naibu wa chifu, wazee wa mitaa na maafisa wa polisi.
- **Vituo vya kurekebisha**-Kuna haja ya kuwarekebisha walevi na wenye matatizo ya matumizi ya dawa za kulevyta kupitia vituo vya urekebishi.



**Tuungane pamoja
tukomeshe dhuluma
ya kijinsia**